# TAARIFA YA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WALIOAJIRIWA KATIKA UTUMISHI WA UMMA 2025

## 1. UTANGULIZI

Taarifa hii inahusu mafunzo elekezi kwa walimu walioajiriwa katika utumishi wa umma 2025 yaliyotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Nkasi tarehe **08.07.2025**.Wilaya ya **Nkasi** ina jumla ya Shule **142** Kati ya shule hizo. Msingi ni **114**, shule za Sekondari **28.** Wilaya ina jumla ya walimu **1589**, kati ya hao Msingi ni **1120**, Sekondari ni walimu **469** katika mchanganuo ufuatao;

| NA. | WILAYA | NKASI | | |
|---|---|---|---|---|
| | | JINSI | | |
| | IDARA | ME | KE | JML |
| 1. | MSINGI | 794 | 326 | 1120 |
| 2 | SEKONDARI | 374 | 95 | 469 |
| JUMLA | | 1168 | 421 | 1589 |

**(Jedwali Namba 1; Idadi ya Walimu Wilaya ya Nkasi)**

## 2. LENGO LA MAFUNZO

Lengo la mafunzo haya ni kutoa elimu kwa walimu wapya **104** walioajiriwa **Wilaya ya Nkasi** katika utumishi wa umma mwaka 2025 kuhusiana na masuala ya nidhamu hasa ukizingatia kuwa walimu wengi wanakosa uelewa wa kutosha kuhusu taratibu za kiutumishi, miiko ya kazi na maadili ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.

## 3. IDADI YA WALIMU WALIOSHIRIKI MAFUNZO ELEKEZI TAREHE 08/07/2025

Katika mafunzo haya jumla ya walimu walioajiriwa katika utumishi wa umma 2025 na kushiriki mafunzo haya elekezi wenye taaluma ya ualimu na ambao hawana taaluma ya ualimu ni kama ifuatavyo:

| Halmashauri | Idara | Idadi ya Walimu wenye taaluma ya Ualimu | | | Idadi ya Walimu wasiokuwa na taaluma ya Ualimu | | | Jumla kuu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| NKASI | MSINGI | 25 | 03 | **28** | - | - | **-** | 25 | 03 | **28** |
| | SEKONDARI | 33 | 24 | **57** | 11 | 07 | **18** | 40 | 35 | **75** |
| **JUMLA KUU** | | **58** | **27** | **85** | **11** | **07** | **18** | **65** | **38** | **103** |

**(Jedwali Namba 2.Idadi ya Walimu walioshiriki mafunzo elekezi)**



*Pichani: Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi (**Bi. Valeliana Mwapasi**-aliyesimama) akifungua semina ya mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya Wilaya ya Nkasi.*

## 4. MADA ZILIZOWASILISHWA

i. Maana,Muundo na Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu
ii. Sheria kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wa umma na utumishi wa walimu
iii. Taratibu za Ajira na Maendeleo ya walimu
iv. Haki na wajibu wa mwalimu
v. Maadili na nidhamu kwa walimu
vi. Taratibu za mawasiliano serikalini na ushughulikiaji wa malalamiko kwa walimu.

Maana,Muundo na Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Katibu Msaidizi Tume ya Utumishi wa Walimu alieleza kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu ni chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu,2016 Sura ya 448 na kuelezea pia muundo wa tume na majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Kifungu cha 5(a)-(l) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, na Kifungu cha 12(1)(a-h) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Sura ya 448.



*Pichani; Katibu Msaidizi (**Bw. Richard M. Katyega**) akiwasilisha mada ya Maana, Muundo na Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu.*

Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa umma; Katika kipengele hiki Afisa Utumishi na Utawala alielezea kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma,Sura 298 na Kanuni zake za mwaka 2022,kuhusiana na masuala ya ajira,mkataba wa utendaji kazi,ukomo wa ajira,nidhamu,rufaa,mafao na mengineyo.

Pia akaelezea kuhusu Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma Toleo la 2009 zinazoelezea taratibu mbalimbali za kiutumishi katika utumishi wa umma.



*Pichani; Afisa Utumishi na Utawala (**Bw. Emmanuel I. Shombe**) akiwasilisha mada ya Sheria kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wa umma.*

Pia Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu alieleza kuhusu masuala ya ajira na maendeleo ya walimu kwa kupitia Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu,Sura 448 na Kanuni zake za Mwaka 2016 zinazohusu mchakato wa ajira na usajili wa walimu, kuthibitisha kazini walimu, kupandishwa vyeo, kubadilishiwa vyeo/kada, mafunzo kazini,Hitimisho la kazi ya Ualimu, kuajiriwa upya katika Utumishi wa Ualimu na Majukumu ya Kazi ya Ualimu.



*Pichani; Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu (**Bi. Yusta J. Luoga**) akiwasilisha mada ya mchakato wa ajira kwa Walimu*

Haki na Wajibu wa Mwalimu; Mada hii iliwasilishwa na Afisa Elimu Divisheni ya Sekondari ambapo pamoja na mambo mengine alielezea kuhusu haki za mwalimu ambazo ni,

i. Haki za Mwalimu katika masuala ya Ajira
ii. Haki za Mwalimu katika Likizo
iii. Haki zinazoambatana na Uhamisho
iv. Haki ya Fidia ya Kuumia Kazini
v. Haki ya Kupata Mikopo
vi. Haki ya Matibabu

vii. Haki ya Gharama za Mazishi na nyinginezo

Pia alielezea wajibu wa mwalimu katika kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika mkataba wake wa kazi **Sehemu 'B' ukurasa wa 5-6 wa Mkataba wa Ajira.**



*Pichani; Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Sekondari (**Bi. Dafrosa F. Mkenda-aliyesimama**) akiwasilisha mada ya Haki na Wajibu wa Mwalimu.*

Pia katika mada hii inayohusu Haki za Mwalimu, Afisa Elimu Divisheni ya Awali na Msingi alielezea suala la Haki za Mwalimu katika Likizo na akaainisha aina za likizo kama ifuatavyo;

i. Likizo ya Mwaka
ii. Likizo ya Ugonjwa
iii. Likizo ya Dharura au Ruhusa(Special Leave of Absence)

Kama vile, kushiriki tukio la michezo, mazishi ya ndugu wa karibu,kuhudhuria mikutano ya vyama vya wafanyakazi,kushughulikia masuala binafsi

iv. Likizo ya Uzazi
v. Likizo bila Malipo

vi. Likizo ya Masomo
vii. Likizo kabla ya kustaafu
viii. Likizo ya kunoa ubongo(Sabbatical Leave)



*Pichani: Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi (**Bw. Eliud Njogellah**-aliyesimama) akiwasilisha mada inayohusu masuala ya likizo kwa washiriki wa mafunzo.*

Maadili na Nidhamu kwa Walimu; Katika mada hii Afisa anayeshughulikia Nidhamu na Maadili Tume ya Utumishi wa Walimu alielezea Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma, Sheria , Kanuni na Miongozo inayosimamia Maadili katika Utumishi wa Umma, Miiko na Maadili ya kazi ya Ualimu, Nidhamu kwa Walimu,Mamlaka za Nidhamu kwa Walimu,Mchakato wa Mashauri ya Nidhamu kwa Walimu,Taratibu za Ushughulikiaji wa Masuala ya Nidhamu kwa Walimu,Mamlaka za Rufaa katika Utumishi wa Walimu na Taratibu na Masharti ya Rufaa.



*Pichani: Afisa Nidhamu na Maadili (**Bw. Christian N. Tuseko**) akiwasilisha mada inayohusu Maadili na Nidhamu kwa Walimu.*

Taratibu za mawasiliano serikalini na Ushughulikiaji wa Malalamiko kwa Walimu mada iliwasilishwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye alikuwa mgeni mwalikwa, nae akaelezea kwa ufupi maana ya mawasiliano kazini,njia za mawasiliano,mtiririko wa mawasiliano ,sheria na kanuni zinazosimamia Mawasiliano Serikalini na Miiko ya mawasiliano.



*Pichani: Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi (**Bw. Afraha N. Hassan**) akiongea na Walimu wa Ajira kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu ajira na utumishi wao.*

## 5. YALIYOBAINIKA KATIKA MAFUNZO

Katika mafunzo haya mwitikio wa walimu hawa wa ajira mpya ulikuwa mkubwa sana licha ya mazingira ya kijiografia kuwa mbali na eneo yalikofanyikia mafunzo haya na pia licha ya changamoto za usafiri washiriki waliweza kufika kwa wakati na mada zilizokusudiwa kufundishwa zilifundishwa kikamilifu.

Mafunzo haya yaliwajengea uwezo mkubwa wa kujua haki zao za msingi kwa mwajiri na pia wajibu wao kwa jamii na taifa kwa ujumla. Waliuliza maswali mengi yaliyohusu kupata uelewa wa kutosha kuhusiana na viwango vya mishahara kutofautiana hasa kwa walimu wa masomo ya sayansi na biashara na wale waliosoma masomo mengine ya sanaa.

Baada ya mafunzo haya washiriki walionyesha nia thabiti ya kuzingatia masharti yaliyopo katika mikataba yao ya kazi na kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa katika kuleta maendeleo yanayotarajiwa na serikali. Pia watajiepusha na vitendo vitakavyoweza kuwasababisha kuingia katika makosa ya kinidhamu na yale mengine ya kijinai.



*Pichani: Mwalimu wa ajira mpya (**Bi**. **Ester Kipenda Katende**) akiuliza swali linalohusu mawasiliano kazini.*

## 6. MAFANIKIO

Mafunzo haya yamefanikiwa kutokana na Mahudhurio ya washiriki kuwa asilimia mia moja kama ilivyokusudiwa. Pia viongozi wote walioalikwa waliweza kushiriki katika mafunzo haya na kufundisha mada zilizoandaliwa wakiwemo; Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Wakuu wa Divisheni ya Elimu (Msingi na Sekondari), Afisa Utumishi na Utawala na Watendaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Nkasi.

## 7. CHANGAMOTO

Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa zoezi hili la utoaji wa mafunzo kwa walimu wa ajira mpya ni ukosefu wa fedha hali iliyopelekea mafunzo haya kushindwa kufanyika kwa muda wa siku tano kwa kushindwa kumudu gharama za chakula kwa washiriki.

## 8. MAONI NA MAPENDEKEZO

Tunaomba katika uendeshaji wa mafunzo haya fedha iongezwe kwa ajili ya kuwezesha chakula na mahitaji mengine kwa washiriki kwa kupitia wadau mbalimbali wa maendeleo. Na pia tunaipongeza Serikali na wadau wengine wa

maendeleo kwa kuona jambo hili la mafunzo elekezi kwa walimu kuwa lina umuhimu mkubwa katika kuimarisha sekta ya elimu nchini.

## 9. HITIMISHO

Katika kuhitimisha, mafunzo haya yamewezesha walimu wapya kupata maarifa muhimu kuhusu sheria, kanuni, taratibu na maadili ya kazi ambayo yatachangia utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi na uwajibikaji mkubwa.



Pichani: Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi (**wa pili toka kushoto**) akitoa neno la shukrani na kuhitimisha mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya walioajiriwa katika utumishi wa umma Wilaya ya Nkasi mwaka 2025 katika Ukumbi wa Halmashauri mjini Namanyere.



Pichani: Mwalimu wa ajira mpya aliyesimamishwa na mgeni rasmi kama mfano kwa walimu waliovaa mavazi yenye unadhifu (Haiba).





Hizi ni picha za washiriki wa mafunzo elekezi (walimu wa ajira mpya) toka sehemu mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi wakiendelea kupatiwa mafunzo yanayohusiana na utumishi wao.





Hawa ni viongozi wawezeshaji wa Mafunzo Elekezi kwa walimu walioajiriwa katika utumishi wa umma Wilaya ya Nkasi yaliyofanyika tarehe 08/07/2025 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

**Mbele kutoka kushoto**: Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Sekondari, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Katibu Msaidizi Tume ya Utumishi wa Walimu, Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi. (**Nyuma kutoka kushoto)**: Afisa ajira na Maendeleo ya walimu (TSC), Afisa Utumishi na Utawala na Afisa Nidhamu na Maadili wa TSC.